Find this and other free educational resources at http://maktaba.tetea.org

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION

015/1

# ELIMU YA DINI YA KIISLAMU 1

(Kwa Watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shuleni)

Muda: Saa 2 — Jumatatu, 11 Novemba 2013 mchana

## Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C, D na E.
2. Jibu maswali **yote**.
3. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
4. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



Find more free educational resources at:
http://maktaba.tetea.org

Scanned by CamScanner

## SEHEMU A (Alama 10)
## SUNNAH NA HADITH

1. Chagua jibu sahihi katika kipengele (i) – (x) kisha andika herufi yake katika kijitabu chako cha kujibia.

(i) Miongoni mwa sababu zilizoongeza msukumo wa mahitaji ya kukusanya Hadithi ni
   A kuwepo kwa mashindano ya kuhifadhi Hadithi
   B kufuata Sunnah ya Mtume (s.a.w)
   C kufuata rai za maswahaba na makhalifa
   D kuwepo kwa uadui dhidi ya Uislamu
   E kuzuka kwa mitume wa uongo.

(ii) Maswahaba mashuhuri waliopokea hadithi nyingi zaidi ni
   A Abuu Huraira (r.a) na Bi Aysha (r.a)
   B Ibn Abbas na Ali (r.a)
   C Abdalah bin Umar na Abdallah bin Abbas
   D Abubakar (r.a) na Uthman (r.a)
   E Zaid bin Zaid na Abdulrahaman bin A'uf.

(iii) Kauli inayodhihirisha mtazamo potofu kuhusu Sunnah ni pamoja na kuonekana kuwa Sunnah
   A ni mwenendo wa Mtume (s.a.w)
   B ni matendo ya hiari kwa Muislamu kuyafuata
   C ni tafsiri ya maagizo ya Allah (s.w)
   D humfikisha mja katika radhi za Allah (s.w)
   E ndiyo inayotafsiri Qur'an.

(iv) Hadithi za Mtume (s.a.w) zinafahamika hadi hivi leo kwa sababu
   A Mtume (s.a.w) mwenyewe alichukua dhima ya kuzihifadhi
   B Waislamu wa mwanzo waliamriwa waandike hadithi
   C Tabiin walitumia hadithi za Mtume (s.a.w) kutoa fat-wa mbalimbali
   D zilitumika kwa kumuigiza Mtume (s.a.w), kuzihifadhi na baadaye ziliandikwa
   E Muhadithina walifanya kazi kubwa ya kukusanya hadithi.

(v) Kitabu kilichoandikwa katika kipindi cha wafuasi wa maswahaba ni
   A Al-qatadaya
   B Jamiu at-Tirmidh
   C Al-muwatta
   D Sunnan ya An-Nisai
   E Sahihi Bukhar.

(vi) Vitabu sita mashuhuri vya Hadithi vimeitwa Sahihi Sitta kwa sababu vimeandikwa na waandishi
   A waliosafiri masafa marefu katika kukusanya Hadithi
   B waliojizatiti kuutekeleza Uislamu
   C waliohakiki Hadith kabla ya kuziandika
   D waliofanya rejea kwenye kitabu mashuhuri cha Imam Malik
   E walioishi katika kipindi cha Tabi Tabiina.



Find more free educational resources at:
http://maktaba.tetea.org
Scanned by CamScanner

## SEHEMU B (Alama 15)

Find this and other free resources at: http://maktaba.tetea.org

## QUR'AN

2. Chagua kifungu cha maneno kutoka **Orodha B** kinachowiana na kifungu cha maneno kutoka **Orodha A.** Andika herufi ya jibu sahihi pembeni ya namba kutoka orodha A.

| ORODHA A | ORODHA B |
|---|---|
| (i) Na Akakukuta fakiri Akakutajirisha? (93:8). | A. Nguzo ya sita ya imani ya Kiislamu. |
| (ii) Mwenyezi Mungu hakuna mola ila yeye…, msimamia kila jambo… ndiye aliye juu (na) ndiye aliye mkuu. (2: 255). | B. Mwenyezi Mungu yupo karibu na binadamu na mjuzi wa mambo yaliyomo kwenye vifua vya watu. |
| (iii) Na haikuwa kwa mtu kwamba Mwenyezi Mungu anasema naye ila kwa Ilhamu au kwa nyuma ya pazia au kutumwa mjumbe (malaika) naye humfunulia kiasi anachotaka mwenyezi Mungu kwa idhini yake … (42:51). | C. Lipa wema zaidi kuliko uliyofanyiwa. |
| (iv) Ametukuka yule ambaye mkononi mwake umo ufalme wa kila kitu; na kwake mtarejezwa nyote. (36: 83). | D. Allah (s.w) hamdhulumu mja wake. |
| (v) Haitakifikia batili mbele yake wala nyuma yake kimeteremshwa na mwenye hikima ahimidiwaye (41:42). | E. Madai ya makafiri dhidi ya Mtume (s.a.w). |
| (vi) Na ukinena kwa sauti kubwa (au ndogo ni sawa sawa) kwani hakika yeye anajua (yaliyo dhahiri na) yaliyo siri na yaliyofichikana zaidi (kuliko siri). (20:7). | F. Watakaoufuata Uislamu watasalimika. |
| (vii) Na kwamba Yeye ndiye anayeleta ya kufurahisha na ya kuliza…afishaye na kuhuisha… aliyeumba dume na jike (la kila kitu)…(53:43-54). | G. Maliwazo kwa Mtume kuwa Mola wake yuko karibu naye sana. |
| (viii) Kwa nini! Sisi tunaweza (hata) kuzisawazisha ncha za vidole vyake (Tutakapomfufua mara ya pili, ziwe kama zilivyokuwa duniani). (75:4). | H. Mambo yatakayosababisha watu kuingia motoni. |
| (ix) Na mwenye kushuhudia na kishuhudiwacho (85:3). | I. Njia anazotumia Allah (s.w) kuwasiliana na waja wake. |
| (x) Na husema: "Oh! Tuiache miungu yetu kwa ajili ya (huyu) mtunga mashairi mwendawazimu?" (37:36). | J. Uwezo wa kipekee wa Allah (s.w). |
| (xi) Na mnapoamkiwa kwa maamkio yoyote yale, basi itikieni kwa yaliyo bora kuliko hayo, au rejesheni yayo hayo. Hakika Mwenyezi Mungu anafanya hisabu ya kila kitu (4:86). | K. Kufufuliwa viumbe ni jambo lisilokuwa na mashaka. |
| (xii) Na wale wanaosema: "Mola wetu! Tuondolee adhabu ya Jahanamu, " bila shaka adhabu yake ni yenye kuendelea. (25:7). | L. Kuwa wanyenyekevu wakati wa kusoma Qur'an. |
| (xiii) Kuwa amali zenu ni mbali mbali; (na jazaa yenu itakuwa mbali mbali) (92: 4). | M. Qur'an imebakia katika asili yake tangu iliposhushwa hadi leo. |
| (xiv) Na anayetaka dini isiyokuwa ya Kiislamu basi haitakubaliwa kwake naye akhera atakuwa katika wenye hasara (kubwa kabisa). (3:85). | N. Namna waja wema wanavyomuelekea Allah (s.w). |
| (xv) … Na wanaposomewa aya zake huwazidishia imani… (8:2). | O. Miongoni mwa matukio ya siku ya hesabu. |
| | P. Kuanza kushuka kwa Qur'an katika mwezi wa Ramadhani. |
| | Q. Suratul Al-ahqaf. |
| | R. Ayatul Kursy. |
| | S. Uwezo wa Allah (s.w) kwa mambo yote. |
| | T. Umuhimu wa elimu. |



Find more free educational resources at:
http://maktaba.tetea.org

Scanned by CamScanner

## SEHEMU C (Alama 15)
## TAWHIID

3. Panga vipengele vya (a), (b) na (c) katika mtiririko wenye kuleta mantinki. Andika herufi na namba tu zinazohusika katika kijitabu chako cha kujibia.

(a) Mwanadamu hawezi kuishi bila ya dini kwa sababu umbile lake ni la kidini, kama ifuatavyo:
- (i) Hakuna mabadiliko katika maumbile ya viumbe vya Mwenyezi Mungu.
- (ii) Ndilo umbile Mwenyezi Mungu alilowaumbia watu.
- (iii) Lakini watu wengi hawajui.
- (iv) Basi uelekeze uso wako katika dini iliyo sawasawa.
- (v) Hiyo ndiyo dini iliyo haki.

(b) Waislamu wanawakubali mitume wote waliokuwa kabla ya Muhammad (s.a.w), kama ilivyojitokea katika Qur'an (2 :286).
- (i) Mola wetu usitutese kama tukisahau (tukaacha yaliyo mema) au tukikosa (tukafanya mabaya).
- (ii) (Faida ya) yale iliyoyachuma (hiyo nafsi) ni yake na hasara ya yale iliyoyachuma ni juu yake.
- (iii) Mwenyezi Mungu haikalifishi nafsi yoyote ila yaliyo sawa na uweza wake.
- (iv) Mola wetu usitutwike tusiyoyaweza na utusamehe, na utughufirie, na uturehemu.
- (v) Mola wetu na usitubebeshe mzigo kama uliowabebesha wale waliokuwa kabla yetu.

(c) Mitume kabla ya Muhammad waliletwa ulimwenguni kama ifuatavyo:
- (i) Yunus (as) kisha Zakaria (as).
- (ii) Suleiman (as) kisha Il-yassa (as).
- (iii) Yahya (as) kisha Issa (as).
- (iv) Harun (as) kisha Al- yasaa (as).
- (v) Dhulkifl (as) kisha Daud (as).



Find more free educational resources at:
http://maktaba.tetea.org
Scanned by CamScanner

Find this and other free resources at: http://maktaba.tetea.org

## SEHEMU D (Alama 30)

## FIQH

4. Jibu maswali yafuatayo kwa kifupi kwa kuandika majibu yako katika kijitabu chako cha kujibia.

(a) Kwa mujibu wa Hadith Sahihi za Mtume (s.a.w), bainisha sifa nne za mnafiki.

(b) Ainisha lengo la ujumla la nguzo za Uislamu.

(c) Taja nguzo nne za kutayammamu.

(d) Khushui (unyenyekevu) hupatikana katika swala kwa kuzingatia mambo gani ? Taja mambo mawili.

(e) Kwa kutumia mnyama kama ngamia, eleza maana ya Nisaab.

(f) Katika jamii yetu lengo la Zakat halifikiwi kwa sababu wengi hawatekelezi masharti ya utoaji. Taja masharti manne tu ya utoaji Zakat.

(g) Eleza tofauti iliyopo kati ya kuhiji na kufanya U'mra.

(h) Kwa mujibu wa mafundisho ya Uislamu, taja mambo mawili yanayomfanya mwanamke asiruhusiwe kufunga.

(i) Tunajifunza nini kutokana na vazi la Ihram linalovaliwa wakati wa Hija na uchungaji wa masharti ya Ihram ?

(j) Orodhesha matendo mawili ya Hija yanayowaunganisha wasiokwenda Hija kiroho na mahujaji.

(k) Ili ndoa iweze kufungika Kiislamu, kuna mambo yanayotakiwa kuwepo. Taja mambo manne tu.

(l) Eleza tofauti iliyopo kati ya muda wa Eda ya kufiwa na Eda ya kuachwa.

(m) Elezea tofauti iliyopo kati ya kuswali na kusimamisha swala.

(n) Katika sheria ya Kiislamu makosa yamegawanyika katika aina tatu. Taja aina mbili.

(o) Kwa kuzingatia mtazamo wa Uislamu, orodhesha mambo mawili yanayofanya wanawake na wanaume wawe na hadhi na haki sawa.



Find more free educational resources at:
http://maktaba.tetea.org

Scanned by CamScanner

Find this and other...

## SEHEMU C (Alama 15)
## TAWHIID

3. Panga vipengele vya (a), (b) na (c) katika mtiririko wenye kuleta mantinki. Andika herufi na namba tu zinazohusika katika kijitabu chako cha kujibia.

(a) Mwanadamu hawezi kuishi bila ya dini kwa sababu umbile lake ni la kidini, kama ifuatavyo:
   (i) Hakuna mabadiliko katika maumbile ya viumbe vya Mwenyezi Mungu.
   (ii) Ndilo umbile Mwenyezi Mungu alilowaumbia watu.
   (iii) Lakini watu wengi hawajui.
   (iv) Basi uelekeze uso wako katika dini iliyo sawasawa.
   (v) Hiyo ndiyo dini iliyo haki.

(b) Waislamu wanawakubali mitume wote waliokuwa kabla ya Muhammad (s.a.w), kama ilivyojitokea katika Qur'an (2 :286).
   (i) Mola wetu usitutese kama tukisahau (tukaacha yaliyo mema) au tukikosa (tukafanya mabaya).
   (ii) (Faida ya) yale iliyoyachuma (hiyo nafsi) ni yake na hasara ya yale iliyoyachuma ni juu yake.
   (iii) Mwenyezi Mungu haikalifishi nafsi yoyote ila yaliyo sawa na uweza wake.
   (iv) Mola wetu usitutwike tusiyoyaweza na utusamehe, na utughufirie, na uturehemu.
   (v) Mola wetu na usitubebeshe mzigo kama uliowabebesha wale waliokuwa kabla yetu.

(c) Mitume kabla ya Muhammad waliletwa ulimwenguni kama ifuatavyo:
   (i) Yunus (as) kisha Zakaria (as).
   (ii) Suleiman (as) kisha Il-yassa (as).
   (iii) Yahya (as) kisha Issa (as).
   (iv) Harun (as) kisha Al- yasaa (as).
   (v) Dhulkifl (as) kisha Daud (as).



Find more free educational resources at:
http://maktaba.tetea.org

Scanned by CamScanner

Find this and other free educational resources at http://maktaba.tetea.org

## SEHEMU E: (Alama 30)
## TAREKH

Chagua **neno** au **vifungu vya maneno** (i) – (xxx) ili kukamilisha kauli (a) – (o) kwa usahihi. Maneno au vifungu vya maneno vinaweza kutumika zaidi ya mara moja.

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| (i) | Khalifa | (ii) | Mtoto | (iii) | Kutubia |
| (iv) | Liwati | (v) | Firauni | (vi) | Ilham |
| (vii) | Jahara | (viii) | Muujiza | (ix) | Ismaili (a.s) |
| (x) | Mussa (a.s) | (xi) | Allah (s.w) | (xii) | Wamemuasi |
| (xiii) | Ad | (xiv) | Aliangamia | (xv) | Yusuf (a.s) |
| (xvi) | Uungu | (xvii) | Mfalme Namrudh | (xviii) | Siri |
| (xix) | Ibilis | (xx) | Kuswali | (xxi) | Uharamia |
| (xxii) | Baba yake | (xxiii) | Mkewe | (xxiv) | Alaaniwe |
| (xxv) | Kusoma Qur-an | (xxvi) | Njama | (xxvii) | Ibrahim (a.s) |
| (xxviii) | Upepo mkali | (xxix) | Elimu | (xxx) | Maghfira |

**Maswali**

(a) Allah (s.w) alimuandaa Mtume (s.a.w) katika njia kuu mbili nazo ni __________ na __________.

(b) Hadhi ya mwanadamu hapa ulimwenguni ni __________ wa __________.

(c) Kibri ni tabia iliyomfanya __________ __________ na Allah (s.w).

(d) Mfano mzuri aliouonesha Nabii Adam (a.s) na mkewe ni pale walipobaini kuwa __________ Mola wao, waliomba __________ haraka.

(e) Kutangaza ujumbe kwa __________, kelele na kwa __________ ni mbinu alizozitumia Nabii Nuhu (a.s) kuwaita watu wake warejee kwa mola wao.

(f) Hatanusurika mtu muovu na adhabu ya Allah (s.w) kutokana na nasaba au hadhi aliyonayo katika jamii; ndio maana __________ na __________ wa Nabii Nuhu (a.s) ni miongoni mwa waliogharikishwa.

(g) Watu wa __________ waliangamizwa kwa __________ kutokana na ushirikina wao.

(h) Allah (s.w) aliyemsamehevu aliwapa makafiri wa kaumu ya Thamud siku tatu baada ya kumuua ngamia wa __________ wapate kuamini na __________.

(i) Nabii Ibrahim (a.s) aliufikisha ujumbe wa Mwenyezi Mungu kwa __________ aliyekuwa mkuu wa ibada za masanamu na __________ kiongozi wa jamii aliyejipa Uungu.

(j) __________ alipomuelekea Mola wake kuomba mtoto atakayemsaidia kazi ya kuhuisha Uislamu alipewa __________ baada ya kumuoa Hajira aliyekuwa mjakazi wa mkewe.

(k) __________ na __________ ni uovu uliopelekea kuangamizwa kwa watu wa Nabii Lut.

(l) Wivu wa ndugu zake Nabii __________ uliwasababisha kubuni __________ za kutaka kumuua.

(m) Pamoja na kuwa Nabii __________ alizaliwa kipindi ambacho __________ aliamrisha watoto wa kiume wauwawe, lakini alilelewa na kukuzwa nyumbani mwake.

(n) __________ aliangamizwa kutokana na neno lake la kujitangazia __________ na kibri dhidi ya ujumbe aliopelekewa kupitia kwa Mussa (a.s) na Harun (a.s).

(o) Kusimama usiku kwa ajili ya __________ na __________ kwa mazingatio ni miongoni mwa kanuni za awali za kusimamisha Uislamu katika jamii alizopewa Mtume (s.a.w).



Find more free educational resources at:
http://maktaba.tetea.org
Scanned by CamScanner